# Injili za Siri: Kuna maandiko ya siri kuhusu Yesu?

***Kweli ni historia ya Yesu?***

Mwaka 1945 ugunduzi ulifanyika nchini Misri ya Juu, karibu na mji wa Nag Hammadi. Nakala hamsini na mbili za maandiko ya kale, yaliyoitwa Injili za siri yalionekana katika vitabu 13 vya ngozi vilivyoandikwa kwa mkono. Yaliandikwa kwa lugha ya Kikoptiki iliyokuwa maktaba katika Jumba la Utawa.

Wasomi wachache wa maandiko hayo ya siri wameenda mbali kudai kwamba maandiko haya yaliyogunduliwa hivi karibuni ni historia yakini ya Yesu badala ya Agano Jipya. Je, imani yao katika maandiko haya inaendana pamoja na ushahidi wa kihistoria? Hebu tuangalie kwa kina kuona kama tunaweza kutenganisha ukweli kutoka katika kubuni.

## “Wajuaji” wa siri

Injili za Siri zinahusishwa katika kikundi kijulikanacho kama (shangazo kubwa hapa) Wajuaji wa siri. Jina lao linatoka katika neno la kigiriki, linamaanisha “maarifa”. Watu hawa walifikiria walikuwa na siri, ufahamu maalumu uliojificha kwa watu wa kawaida.

Kwa kadri ukristo ulivyoenea, Wanostiki (Wajuaji wachache) walichanganya imani baadhi na masuala ya ukristo kwenye imani zao, wakibadili Unostiki (Usiri) kuwa ukristu bandia. Labda walifanya hivyo kuongeza idadi ya washirika na kumfanya Yesu mtoto wa matangazo kwa sababu zao. Vile vile, kwa mfumo wao wa fikra kuendana na ukristu, Yesu alihitaji kuelezewa upya, kuvuliwa yote ubinadamu wake na uungu wake halisi.

Katika historia ya Ukristu ya Oxford, John McManners aliandika mchanganyiko imani za Kinostiki, kikristo na kizushi.

Ujuzi-siri ulikuwa (na bado ni) theosophia (elimu ya Mungu ya kiroho) zenye michanganyiko mingi. Ushirikina na imani za kizushi za kienyeji zilichanganywa na elimu ya nyota, uchawi. … Wakakusanya misemo ya Yesu iliyotengenezwa kufaa tafsiri zao (kama katika Injili ya Thomaso), na wakawapa wafuasi wao fursa au namna ya upinzani wa Ukristu.[1]

## Kosozi za mwanzo

Mazoea kidogo ya falsalfa za siri za wachache yalikuwa tayari yanakua katika karne ya kwanza, miongo kadhaa ya kifo cha Yesu. Mitume katika mafundisho na maandiko yako, walienda mbali kulaumu imani hizi kwamba zimepingana na ukweli wa Yesu, kwake yeye ambaye walikuwa mashahidi wa macho.

Angalia, kwa mfano, kile mtume Yohana aliandika karibu mwisho wa karne ya kwanza:

> Nani ni mwongo mkubwa? Anayesema kwamba Yesu si Kristo. Watu hao ni wapinga Kristo, kwa sababu wamemkana Baba na Mwana. (1 Yohana 2:22, NIV).

Wakifuata mafundisho ya mitume, viongozi wa kanisa la mwanzo kwa pamoja wakalaumu mafundisho ya Kinostiki ya siri ya wachache kuwa ni ya kidhehebu-tenge. Padri wa Kanisa Irenaeus, akiandika miaka 140 kabla ya Baraza la Nicaea, alihakikisha kwamba Wanostiki walilaumiwa na kanisa kama wapinzani. Pia alizikataa “injili” zao. Vile vile, akirejelea kwenye Injili nne za Agano Jipya, alisema, “Haiwezekani kwamba Injili zinaweza kuwa zaidi au chache kwa idadi kuliko zilivyo.”[2]

Mwanateolojia Origen aliandika hili katika karne ya tatu, zaidi ya miaka mia moja kabla ya Nicaea:

> Najua injili fulani ambayo inaitwa “Injili kulingana na Thomaso” na “Injili kulingana na Mathayo”, na nyingi nyinginezo tulizosoma – tusifikiriwe kwa njia yoyote wajinga kwa sababu ya hao wanaofikiri wanamiliki

elimu fulani ikiwa wamejulishwa haya.

Hata hivyo, miongoni mwa yote haya tuliyothibitisha pekee ambayo kanisa limetambua, ambalo ni kwamba Injili nne tu zinapaswa kukubaliwa.[3]

## Watunzi wa Siri

Inapokuja kwenye injili za siri za wachache, karibu kila kitabu kinabeba jina la sifa ya Agano Jipya: Injili ya Philipo, Injili ya Petro, Injili ya Maria, Injili ya Yuda, na kuendelea . Lakini ziliandikwa na watunzi wao waliokusudia? Hebu tuangalie.

Injili za Wanostiki zinawekewa tarehe karibia miaka 100 hadi 300 baada ya Kristo, hakuna msomi wa kuaminika anaamini chochote kati ya hivyo ambavyo vingeweza kuandikwa na wenzi-jina (somo) wao. Katika maktaba ya James M. Robinson's Maktaba ya Nag Hammadi tunajifunza kwamba Injili za Kinostiki za wachache ziliandikwa hasa kwa kiasi kikubwa na watunzi wasiojulikana wasiohusiana.[4]

Msomi wa Agano Jipya Norman Geisler anaandika "Maandiko ya Siri ya Wachache (Wanostiki) hayakuandikwa na mitume, bali na watu katika karne ya pili (na baadaye) wakijifanya kutumia mamlaka ya kitume kuendeleza mafundisho yao wenyewe. Leo tunaita suala hili uongo na uzushi wa kufoji."[5]

## Siri kulinganisha Historia

Injili za Kinostiki (Wachache) si maelezo ya kihistoria ya maisha ya Yesu bali badala yake ni maneno ya wachache, yaliyofichwa katika fumbo-siri, yakiacha/yakiruka maelezo ya kihistoria kama majina, sehemu na matukio. Hii ni kinyume kabisa na Injili za Agano Jipya ambazo zimekusanya maelezo ya kweli yasiyo na idadi kuhusu maisha ya Yesu, idara na maneno.

Nani ungemwamini zaidi – mtu anayesema, "Hey, nimepata habari za siri ambazo zilidhihirishwa kiajabu na kisiri kwangu, au mtu fulani ambaye anasema, nimetafuta ushahidi wote na historia yote na huu hapa ushahidi kwa ajili yako ili uweke akilini. Tukizingatia swali hilo akilini, fikiria kauli mbili zifuatazo, ya kwanza kutoka katika Injili ya Wanostiki (Wajuaji wachache) ya Thomaso (c. 110-150 A.D.) na ya pili kutoka Injili ya Agano Jipya ya Luka (c. 55-70 A.D.).

- Hizi ni kauli zilizofichwa ambazo Yesu anayeishi alizungumza na Yuda Thomaso pacha alirekodi.[6]
- Watu wengi wameandika maelezo kuhusu matukio ambayo yalitokea miongoni mwetu. Walitumia kama vyanzo vyao vya taarifa zinazozunguka miongoni mwetu kutoka katika mitume wa mwanzo na mashahidi wengine wa macho wa kile Mungu amefanya katika kutimiza ahadi zake. Nikiwa kwa makini nimechunguza yote ya maelezo haya tangu mwanzo, nimeamua kuandikia ufupisho makini, kukuhakikishia ukweli ninyi wote mliofundishwa. (Luka 1:1-4, NLT)

Unaiona njia ya wazi dhahiri ya Luka inavyoonekana? Na unajua ukweli kwamba iliandikwa karibu na matukio halisi ili iendane na uhakika wake? Ikiwa ni hivyo, hivyo ndivyo kanisa la mwanzo lilivyofikiria pia.

Na wasomi wengi wanakubaliana na maoni ya kanisa la kale kwamba Agano Jipya ni historia halisi ya Yesu. Msomi wa Agano Jipya Raymond Brown amesema kuhusu Injili za Siri za Wachache, "Tunajifunza si tu ukweli mpya pekee wa kuthibitika kuhusu idara ya Yesu ya kihistoria, na minong'ono michache ambayo inawezekana ikawa yake."[7]

Hivyo, ingawaje maandiko ya siri ya wachache ya kinostiki yamewavutia baadhi ya wanafunzi, tarehe zake za mwisho na utunzi unaopaswa kuhojiwa hauwezi kulinganishwa na Agano Jipya. Tofauti hiyo kati ya Agano Jipya na maandiko ya siri ya wachache wazushi (wanostiki) ya kutisha kwa hao wanaong'ang'ania nadharia ya ushiriki wa hila. Mwanahistoria ya Agano Jipya F.F. Bruce aliandika "Hakuna mkusanyiko wa fasihi za kale duniani unaofaidi utajiri wa uthibitisho mzuri wa maandishi kama Agano Jipya.[8]

## Je ni kweli Yesu alifufuka toka katika Wafu?

Swali kubwa zaidi la wakati wetu “Nani ni Yesu Kristo wa kweli?” Alikuwa tu mtu wa pekee, au alikuwa Mungu katika mwili, kama Paulo, Yohana na wafuasi wake waliomini?

Mashahidi wa macho kwa Yesu Kristo kwa kweli walizungumza na walitenda kama walivyoamini, aliinuka kimwili toka katika wafu baada ya kusulubiwa kwake. Ikiwa hawakuwa sahihi basi Ukristu umejengwa katika uongo. Lakini kama walikuwa sahihi, muujiza huo ungethibitisha yote Yesu alisema kuhusu Mungu, yeye mwenyewe na sisi.

Lakini lazima tuchukue ufufuko wa Yesu Kristo kwa imani pekee, au kuna ushahidi mzito wa kihistoria? Wakosoaji wachache walianza uchunguzi kwenye rekodi za kihistoria kuthibitisha maelezo ya ufufuko ni uongo. Ni kitu gani waligundua?

Bonyeza hapa kwa ajili ya kudai zaidi fantastic milele alifanya - ya ufufuo wa Yesu Kristo!

## Ni kweli Yesu alifufuka toka katika Wafu?

Mashahidi wa macho kwa Yesu Kristo kwa kweli walizungumza na walitenda kama walivyoamini, alifufuka toka katika wafu baada ya kusulubiwa kwake. Ikiwa walikosea basi uKristu umeanzishwa kwa uongo? Lakini kama walikuwa sahihi, muujiza huo ungethibitisha yote Yesu aliyosema kuhusu Mungu, kuhusu yeye na kutuhusu sisi.

Lakini ni lazima tuamini ufufuko wa Yesu Kristo kwa imani pekee, au kuna ushahidi wowote wa kihistoria? Wakosoaji kadhaa walianza uchunguzi kwenye kumbukumbu za kihistoria kujaribu kuona kama kweli maelezo ya ufufuko yalikuwa uongo. Kitu gani waligundua?

Kuangalia ushuhuda wa madai makuu yaliyowahi kufanyika ya ufufuko wa Yesu Kristo!

Bonyeza hapa kwa ajili ya kudai zaidi fantastic milele alifanya – ya ufufuo wa Yesu Kristo!